JAMHURI UK11.



# Bei chakula cha kuku yapaa





Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega

**DAR ES SALAAM**

NA MBARAKA **KAMBONA**

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo wamejipanga kuhakikisha malighafi za kutengenezea chakula cha kuku ikiwamo mahindi na soya vinapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu ili kupunguza gharama za uzalishaji baada ya kupanda.

Kauli hiyo aliitoa Dar es Salaam hivi karibuni alipotembelea Kiwanda cha Interchick kuona shughuli za uzalishaji wa chakula cha kuku na ututoleshaji wa vifaranga.

"Kwa upande wa chakula cha kuku tumejipanga kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, wachakataji na wauzaji wa chakula cha kuku kutafuta suluhu ya jambo hili, hatutaki kuona mahindi na soya vinakuwa ni tatizo kwa wachakataji na wauzaji wa chakula cha kuku," amesema.

Pia amesema wanataka kuwapa kipaumbele wadau hao kwa sababu tasnia hiyo ina uwezo wa kuajiri watu wengi na kuzalisha chakula cha kutosha chenye uhakika wa protini kitakachosaidia kujenga jamii yenye afya bora na nguvu.

Katika jitihada za kutatua changamoto zinazoikabili tasnia hiyo, amesema wanakusudia kukutana na wadau wote wanaojihusisha na mnyororo wa thamani wa zao la kuku ili kujadiliana na kuweka mipango madhubuti ya kutatua changamoto zao ili waweze kufanya shughuli zao kwa gharama nafuu na wapate faida.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, amemueleza Ulega kuwa wametenga Sh bilioni 3.9 kutoka katika asilimia 10 ya mfuko wa kuwezesha vijana, kina mama na watu wenye ulemavu ili kuwezesha vikundi vya ujasiriamali.

"Sisi Wilaya ya Kinondoni tumetenga kiasi kisichopungua Sh milioni 150 kutoka katika asilimia 10 iliyotengwa kuwawezesha wajasirimali na tutawapatia vikundi vinane vya wafugaji wa kuku," amesema.

Awali, Mkurugenzi wa Kampuni ya Interchick, Nelson Kikolea, amesema upatikanaji wa nafaka ya mahindi na soya umekuwa ni changamoto kubwa na kusababisha gharama za uzalishaji kuongezeka na wanaoathirika zaidi ni wafugaji wadogo wadogo.

Amesema kuwa bei ya mahindi mwaka jana ilikuwa Sh 460 kwa kilo moja lakini mwaka huu imepanda hadi Sh 940 kwa kilo moja, ikiwa ni ongezeko la Sh 480.

# Ndani ya Habari

**SENSA:** Manufaa ya sensa ni zaidi ya udhaniavyo **UK 8**

**ELIMU:** Makosa ya kuepuka wakati wa kuomba kozi vyuo vikuu **UK 13**

# Siku 3 za DPP kuwajibu wafugaji

**Wadai mifugo yao ilivunja boma, wakaitafuta kwa siku 12. Wanapinga mifugo kutakiwa kuuzwa kwa mnada kufidia gharama za wakulima walioharibiwa mazao yao**

Daniel Mjema, Mwananchi
dmjema@mwananchi.co.tz



Baadhi ya mifugo kati ya 1,450 iliyokamatwa katika mashamba ya wakulima eneo la West Kilimanjaro wilayani Siha mkoani Kilimanjaro. Picha ya Maktaba

**Moshi.** Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) amepewa siku tatu kuwasilisha majibu kinzani ya kiapo cha wafugaji wawili ambao wameweka zuio la kuuzwa kwa mnada kwa mifugo yao 1,448 iliyokamatwa wilayani Siha wiki mbili zilizopita.

Wakati Jaji Safina Semfukwe wa Mahakama Kuu kanda ya Moshi akitoa amri hiyo jana, wafugaji hao, wameeleza katika hati ya kiapo kuwa mifugo yao hiyo ilivunja boma walikokuwa wamehifadhiwa Julai 2, 2022 na kuelekea kusikojulikana.

Ng'ombe hao 485 na jumla ya kondoo na Mbuzi 963, walikuwa wauzwe kwa mnada jana kwa amri ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Siha, iliyotolewa Julai 12, 2022 kabla ya kuzuiwa na Mahakama Kuu kutokana na maombi ya wafugaji hao.

Jana maombi ya wafugaji hao wanaotetewa na wakili Elia Kiwia, yalitajwa mbele ya Jaji Simfukwe ambaye alimtaka DPP na mjibu maombi wa pili, Newton Makwale kuwasilisha kiapo kinzani ndani ya siku tatu na kesi itatajwa Julai 21.

Hata hivyo, idadi ya mifugo inayoonekana kwenye hukumu ya Hakimu Mkazi Siha, Jasmin Abdul ya 1,448 kwa maana ya ng'ombe 485 na mbuzi na kondoo 963, inatofautiana na iliyopo kwenye hati ya kiapo ya mbuzi 1,300 na ng'ombe 485.

## Walichoeleza wafugaji

Katika hati ya kiapo chao, wafugaji hao, Sinjore Laizer na Isaya Mollel wameieleza mahakama kuwa wao ndio wamiliki wa mbuzi 1,300 na ng'ombe 485 ambao maombi ya kuwataifisha yaliwasilishwa mahakama ya Siha na kutolewa uamuzi.

Wanaeleza kuwa Julai 2, 2022, huko nyumbani kwao Lerai wilaya ya Longido, mifugo iliyotajwa ilivunja uzio wa eneo walimokuwa wanatunzwa na kwenda kusikojulikana na jitihada za wanakijiji kuwatafuta hazikuzaa matunda.

Kupitia kwa wakili Kiwia, wanadai baada ya siku mbili tangu kutoweka kwa mifugo yao, walikwenda kutoa taarifa kituo cha Polisi cha Olmolog lakini wakawaambia wanaweza kuwa wamechanganyika na makundi mengine ya mifugo.

Wafugaji hao wanaeleza polisi hao waliwataka waendelee kutafuta mifugo yao na Julai 13, 2022 walikwenda kituo cha Polisi Sanyajuu kuulizia kama wameiona mifugo hiyo na waliwaambia ilipatikana na inahifadhiwa shamba la Narco Siha.

Wanaeleza katika kiapo hicho kuwa, polisi hapo waliwaeleza kuwa baada ya mifugo hiyo kukutwa ikirandaranda katika mashamba ya milimani huko West Kilimanjaro, walimjulisha mjibu maombi wa kwanza (DPP) kwa hatua zaidi.

Kulingana na kiapo hicho, wafugaji hao wanasema polisi hao walienda mbali na kuwajulisha kuwa suala hilo lilishafunguliwa shauri mahakama ya Hakimu Mkazi Siha na kutolewa uamuzi kuwa mifugo hiyo iuzwe kwa mnada wa hadhara.

Wafugaji hao wanadai kulikuwapo na ukiukwaji wa taratibu za kisheria, hivyo Mahakama Kuu ilipaswa kuingilia kati na kwamba hawakupewa haki ya asili ya kusikilizwa na hivyo ili kutenda haki, ni vyema na wao wakasikilizwa.

"Tuko tayari kuweka dhamana au wadhamini kwa masharti yatakayowekwa na mamlaka yoyote ili mifugo iachiwe na kuwa chini ya uangalizi wetu katika kipindi chote cha uchunguzi wa suala hilo,"walisema.

> **"'Tuko tayari kuweka dhamana au wadhamini kwa masharti yatakayowekwa na mamlaka yoyote ili mifugo iachiwe na kuwa chini ya uangalizi wetu..."**
>
> Mmoja wa wafugaji

## Maombi ya DPP yalivyokuwa

Mara baada ya kukamatwa kwa ng'ombe hao, DPP akiwakilishwa na wakili mwandamizi wa Serikali, Kassim Nassir akisaidiwa na mwendesha mashitaka, David Chishimba walifungua maombi ya jinai namba 17 ya mwaka 2022.

Katika maombi hayo yaliyosikilizwa na Hakimu Mkazi Siha, Jasmin Abdul, waliomba mambo mawili, moja ni mahakama itoe amri ya kukamatwa, kuzuiwa na kutaifishwa kwa ng'ombe 485 na mbuzi na kondoo wapatao 963.

Pia wakaiomba mahakama iteue dalali wa kuuza kwa mnada wa dharura mifugo hiyo na kwamba fedha zitakazotokana na mauzo hayo ziingizwe katika akaunti yenye jina la DPP iliyopo katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Akiwasilisha hoja za maombi hayo, wakili Nassir alisema mifugo hiyo iliingizwa kwa jinai katika mashamba ya wakulima katika kijiji cha Olmolog na kwamba mbali na kuingizwa kwa jinai, ilikiuka sheria udhibiti magonjwa ya wanyama.

Wakili Nassir alisema mifugo hiyo inatoka nje ya wilaya ya Siha na mkoa wa Kilimanjaro na iliingizwa katika mkoa huo bila vibali vya maofisa mifugo kwa mujibu wa sheria ya magonjwa ya mifugo ya mwaka 2003.

Mbali na hoja hiyo, lakini alisema mifugo ililishwa katika mashamba ya wakulima yenye mazao aina ya njegere, ngano, mbaazi na mazao mengine na kwamba hadi anawasilisha maombi hayo, hakuna aliyejitokeza na kudai kuwa ilikuwa ni mifugo yake.

Wakili Nassir aliieleza mahakama kuwa mifugo hiyo ilikuwa inahifadhiwa katika shamba la Ranchi ya Taifa (Narco) wilayani Siha ambalo halina miundombinu ya kutosha na wafanyakazi na inaweza ikafa kwa kukosa huduma endelevu.

"Waathirika (wakulima) ambao mazao yao yaliharibiwa wanategemea kuuzwa kwa mifugo hiyo ili waweze kufidia hasara waliyoipata,"alieleza wakili huyo.

Akitoa uamuzi wake, Hakimu Jasmin alisema alifika eneo inapotunzwa mifugo hiyo na kushuhudia yale aliyoyasema wakili Nassir na kuongeza kuwa ameshuhudia eneo hilo linakabiliwa na ukame.

Hakimu huyo alisema ukame huo unaweza kusababisha ng'ombe kufa kama hatua za haraka hazitachukuliwa.

Kwa mujibu wa hakimu huyo, hadi anapoandika uamuzi huo Julai 12, hakuna mtu aliyekuwa amejitokeza kudai kuwa ni mmiliki halali.

Hakimu Jasmin alitoa amri ya kutaifishwa mifugo hiyo na akamteua Newton Makwale kuwa dalali wa kuiuza kwa dharura na fedha zitakazopatikana ziingizwe kwenye akaunti ya DPP iliyopo BoT.

### USULI

**Awali Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai aliagiza kukamatwa mifugo 1,450 iliyoingizwa kwenye mashamba ya wakulima eneo la West Kilimanjaro, Wilaya ya Siha ambayo iliharibu zaidi ya ekari 1,800 za ngano na maharage.**

**Kagaigai alichukua hatua hiyo Julai 10, 2022 baada ya wafugaji hao ambao wanadaiwa kuwa ni jamii ya Kimasai kuwavamia baadhi ya wakulima usiku na kuwajeruhi kwa kuwakata mapanga wakati wakizuia mifugo hiyo kutoingia kwenye mashamba yao.**

**Baadaye iliamriwa mifugo hiyo iuzwe kabla ya wamiliki wake kwenda Mahakama Kuu kupinga amri hiyo.**

**Julai 2**

Siku mifugo hiyo ilipotoweka

CamScanner

UHURU UK 21

# ...sukari unaongezeka

limo
...ora,

lima
cha
...egu

...amia
...ama
...bele
...noto
...geza

wa
...ezaji,
...miliki
...ukari,
kwa

...ukari,
...sema
...kisha
...alika
na
...e.



# Waziri ahimiza ufugaji ng'ombe wa kibiashara

**Na SCOLASTICA MSEWA,** *Chalinze*

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka wafugaji wa ng'ombe kuacha ufugaji kwa imani za kiasili, ambazo zinasababisha ugumu wa kufikia mafanikio katika sekta ya ufugaji.

Ndaki aliyasema hayo juzi, katika uzinduzi wa maonyesho ya mifugo kibiashara yaliyofanyika Chalinze mkoani Pwani ambayo yaliandaliwa na Chama cha wafugaji Ng'ombe kibiashara (TCCS).

Alisema shughuli za mifugo na uvuvi nchini

> **Sekta ya mifugo ni kipaumbele katika Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, ili kuhakikisha inachangia wananchi kutoka katika umasikini na upatikanaji malighafi za viwanda vya kusindika na kuchakata mazao ya mifugo.**
>
> Mashimba Ndaki.

zinafanyika kwa kuhusisha [illegible] ya kiasili, wakati sekta hiyo inahitaji ujuzi na teknolojia.

"Sekta ya mifugo ni kipaumbele katika Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, ili kuhakikisha inachangia wananchi kutoka katika umasikini na upatikanaji malighafi za viwanda vya kusindika na kuchakata mazao ya mifugo,"alieleza.

Alisema Serikali inaendelea na utekelezaji wa mfumo wa kielektroniki kuweka alama za mifugo badala ya kutumia chapa ya moto, lengo ni kuongeza upatikanaji ngozi zenye ubora.

Naye, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alikipongeza chama hicho kwa kuwa ni wadau muhimu ambao wametimiza ndoto ya Serikali ya kuwaweka pamoja wafugaji nchini.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa TCCS, Naweed Mulla, alisema chama hicho kinachounganisha wafugaji wa ng'ombe kibiashara, wamejikita katika kuzalisha na kuuza ng'ombe wenye tija.

UHURU UK 16.

# Malima ataka ng'ombe walionona Nanenane

**Na LATIFA GANZEL** *Morogoro,*

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, amewataka washiriki wa maonyesho ya wakulima Nanenane Kanda ya Mashariki, kupeleka bidhaa zenye ubora wakiwemo wanyama wenye viwango bora.

Maonyesho ya Nanenane yanatarajiwa kufunguliwa Agosti Mosi, mwaka huu na yanafanyika mkoani Morogoro, katika viwanja vya Julius Nyerere.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha maandalizi ya Nanenane Kanda ya Mashariki, inayoundwa na mikoa minne ya Dar es salaam, Pwani, Tanga na Morogoro.

"Wanaoleta wanyama katika 'zoo' walete simba na wanyama wengine walionona, kuna wakati aliletwa simba kakondeana unajisikia aibu kumwangalia,"alisema Malima.

Mkuu huyo wa mkoa alisema katika maonyesho hayo watoto wataingia bura na wazazi walioambatana nao watalipa kiingilio sh.1000 mtu mmoja.

"Hadi sasa maandalizi yote yamekamilika, bustani ziko vizuri, mashirika, taasisi za serikali na binafsi yanayotarajiwa kushiriki ni zaidi ya 500,"alisema.

Mkuu huyo alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kuchangamkia fursa za elimu na teknolojia bora ya kilimo cha kisasa, ili kupata mavuno stahiki na kujikwamua kiuchumi.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro,Albert Msando, aliwataka wananchi wa wilaya hiyo na maeneo mengine kufika katika Banda la Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, kuona wakulima wa mijini watakavyotumia ardhi kidogo ya kulima kwa tija.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Kilimo wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Michael Waluse, alisema kuna umuhimu wa wakulima kutumia teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone ya maji, ili kutunza na kuhifadhi maji kwa matumizi mengine ya kibinadamu.

**Kilimo**

**MAONYESHO**

Maonyesho ya Nanenane yanatarajiwa kufunguliwa Agosti Mosi, mwaka huu na yanafanyika mkoani Morogoro, katika viwanja vya Julius Nyerere.

CamScanner